Injili Kama Alivyoiandika Isaya

na

Ellis Forsman

Injili Kama Alivyoiandika Isaya

na

Ellis Forsman

Oktoba 7, 2011

Injili Kama Alivyoiandika Isaya

Isaya 1:1

Bila shaka umeshawai kusikia kuhusu injili nne...

- Injili kama Alivyoiandika Mathayo.
- Injili kama Alivyoiandika Marko.
- Injili kama Alivyoiandika Luka.
- Inlili kama Alivyoiandika Yohana.

Lakini je umeshawai kusikia injili kama alivyoiandika Isaya.

Kuhubiri injili ya Kristo, haikuwa jambo la kawaida kwa mitume na wengine katika karne ya kwanza ukizingatia Agano la kale.

Ilikuwa ni desturi ya Paulo. Matend 17:2-3, *"Na Paulo kama ilivyokuwa desturi yake, akaingia mle walimo akahojiana nao ka maneno ya maandiko sabato tatu, akiyafunua na kuwaeleza ya kwamba, ili mpasa Kristo kuteswa na kufufuka katika wafu, nay a kwamba Yesu huyu ninaye wapasha habari zake ndiye Kristo."*

Apolo naye alifanya hivyo kule Korintho. Matend. 18: 27-28, *"Na alipotaka kuvuka bahari aende mpaka Akaya, ndugu wakawaimiza, wakawaandikia wale wanafunzi wanafunzi wamkaribishe, naye alipofika akawasaidia sana wale waliokwisha kuamini kwa neema ya Mungu. Kwa maana aliwashinda Wayahudi kabisa kabisa mbele ya watu wote, akionyesha kwa maneno ya maandiko ya kuwa Yesu ni Kristo."*

Hiyo ilikuwa ni kwa sababu ya dalili zilizoonekana ya injili ambayo tayari ili tabiriwa na manabii wa Agano la kale...

- Kuhusu kuja kwa Masihi (Yesu Kristo).
- Kuhusu kuanzishwa kwa ufalme wake.

Nabii kama huyo alikuwa Isaya, aliyeishi miaka 750 kabla ya Yesu Kristo; aliyetumwa kutabiri juu ya Yuda na Yerusalem.

Isa. 1:1, *"Haya ni maono ya Isaya, mwana wa wa Amozi aliyoyaona katika habari za Yuda na Yerusalemu, siku za Uzia na Yothamu na Ahazi na Hezekia, wafalme wa Yuda."*

Kitabu cha Isaya kina unabii mwingi kumhusu Masihi na ufalme wake... mara nyingi ameita "Unabii wa Masihi".

Tunaweza kukiita kitabu chake “Injili kama ilivyoandikwa na Isaya”. Kuelezea pointi yangu, ebu tuangalie unabii mwingine unaopatikana katika kitabu cha Isaya.

Injili ya Masihi

Habari njema kuhusu mwanaume Yesu Kristo.

Atazaliwa na bikira.

Ambaye jina lake litakuwa Emmanueli (“Mungu pamoja nasi”). Isa.7:14, *“Kwa hiyo Bwana mwenyewe atawapa ishara; tazama, bikra atachukua mimba, na kuza mwana, na ataitwa jina lake Emmanueli.”*

Na hiyo ilitimizwa katika kuzaliwa kwa Yesu na Mariamu. Math. 1: 18-23*, “Kuzaliwa kwake Yesu Kristo kulikuwa hivi, Mariamu mama yake alipokuwa ameposwa na Yusufu kabla hawajakaribiana ,alionekana ana mimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu. Naye Yusufu mumewe, kwa vile alivyokuwa mtu wa haki, asitake kumwaibisha aliazimu kumwacha kwa siri. Basi alipokuwa akifiri hayo, tazama malaika wa Bwana alimtokea katika ndoto, akisema Yusufu mwana wa Daudi, usihofu kumchukua Mariamu mkeo maana mimba yake ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu. Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao. Hayo yote yamekuwa ili litimie neno lililonenwa na Bwana kwa ujumbe wa nabii akisema, tazama bikra atachukua mimba, naye atamzaa mwana; nao watamwita jina lake imanueli; yaani, Mungu pamoja nasi.”*

Atakuwa mwana wa ajabu.

Kwa jina la mshangao, aliteuliwa kutawala. Isa.9:6-7*, “Maana kwa ajili yetu motto amezaliwa , tumepewa motto mwanamume; na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake; naye ataitwa jina lake mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, mfalme wa amani. Maongeo ya enzi yake na amani hayatakuwa na mwisho kamwe, katika kiti cha enzi cha Daudi na ufalme wake; kuuthibitisha na kuutegemeza kwa hukumu na kwa haki, tangu sasa na hata milele. Wivu wa BWANA wa majeshi ndio utakaotenda hayo.”*

Hii ilitangazwa na malaika wakati wa kuzaliwa kwa Yesu. Luka 2:11, “*Maana kwenu katika mji wa Daudi amezaliwa mkombozi, ambaye ni Kristo Bwana.”*

Atakuwa kati ya familia ya Daudi (Yese).

Akishuka katika "shina la Yese" (Baba yake Daudi). Isa. 11:1, *"Basi liktoka chipukizi katika shina la Yese na tawi litakalotoka katika mizizi yake litazaa matunda."*

Ukoo wa Yesu unaonyeshwa katika Math. 1(kupitia Yusufu) na Luka 3 (kupitia Maria).

Roho wa Bwana atapumzika juu yake.

Kwa hakima na uelewa, ushauri na utaua, hekima na kumheshimu Bwana. Isa. 11:2, *"Na roho ya BWANA akakaa juu yake, roho ya hekima na ufahamu, roho ya shauri na uwezo, roho ya maarifa nay a kumcha BWANA."*

Hii ilifunuliwa kwa Kutazamwa wakati wa ubatizo wake na Yohana. Math. 3:16, *"Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini, na tazama mbingu zikamfunukia akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua akija juu yake."*

Habari njema kuhusu kazi yake.

Atatanguliwa na anayeandaa njia.

Mmoja aliyetumwa kutengeneza njia. Isa. 40: 3-5, *"Sikiliza ni sauti ya mtu aliaye, itengenezeni nyikani njia ya BWANA; nyosheni jangwani njia kuu kwa Mungu wetu. Kila bonde litainuliwa, na kila mlima na kilima kitashushwa; palipopotoka patakuwa pamenyoka na palipoparuza patasawazishwa; na utukufu wa BWANA utafunuliwa, na wote wenye mwili watauona pamoja; kwa kuwa kinywa cha BWANA kimenena haya."*

Hii ilitimizwa na kazi ya Yohana Mbatizaji. Math. 3:1-3, *"Siku zile aliondokea Yohana mbatizaji akihubiri katika nyika ya Uyahudi na kusema, tubuni kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia. Kwa sababu huyo ndiye aliyenenwa na nabii Isaya akisema, sauti ya mtu aliaye nyikani, itengenezeni njia ya Bwana, yanyosheni mapito yake."*

Atakuwa mpakwa mafuta kuhubiri habari njema.

Kwa masikini, anatangaza mwaka wa Bwana uliyokubaliwa. Isa. 61:1-3, *"Roho wa MUNGU i juu yangu kwa sababu BWANA amenitia mafuta niwahubiri wanyenyekevu habari njema, amenituma ili kuwaganga waliovunjika moyo, kuwatangazia mateka uhuru wao, na hao waliofungwa habari za kufunguliwa kwao. Kutangaza mwaka wa BWANA uliokubaliwa, na siku ya kisasi cha Mungu wetu; kuwafariji wote waliao; kuwaagizia hao waliao katika Sayuni, wapewe taji ya maua badala ya majivu mafuta ya furaha badala ya maombolezo, vazi la sifa badala ya nzito, wapate kuitwa miti ya haki; iliyopandwa na BWANA ili atukuzwe."*

Hii ilitimizwa kwa mahubiri yake kule Nazareti. Luka 4:16-21, *"Akaenda Nazaareti hapo alipolelewa; na siku ya sabato akaingia katika sinagogi kama ilivyokuwa desturi yake akasimama ili asome. Akapewa chuo cha nabii Isaya, akakifungua chuo akatafuta mahali palipoandikwa, Roho wa Bwana yu juu yangu, kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma niwatangazie wafungwa kufunguliwa kwao, na vipofu kupata kuona tena, kuwaacha huru waliosetwa, na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa. Akakifunga chuo akamrudishia mtumishi, akaketi; na watu wote waliokuwamo katika sinagogi wakamkazia macho. Akaanza kuwambia, leo maandiko haya yametimia masikioni mwenu."*

Angeweza kuleta mwanga kwa hao walioishi Galilaya.

Katika mkoa wa Zebuluni na Nafutali. Isa. 9:1-2, *"Lakini yeye aliyekuwa katika dhiki hatakosa changamko. Hapo kwanza aliiingiza nchi ya Zabuloni na nchi ya Naftali katika hali ya kudharauliwa lakini zamani za mwisho ameifanya kuwa tukufu karibu na njia ya bahari; ng'ambo ya Yordani, Galilaya ya mataifa. Watu wale waliokwenda katika giza wameona nuru kuu; wale waliokaa katika nchi ya uvuli wa mauti, nuru imewaangaza."*

Hii ilitimizwa kwa kuishi kwake na kuhubiri Kapernaumu. Math. 4:12-16, *"Basi Yesu aliposikia kwamba Yohana amefungwa alikwenda zake mpaka Galilaya, akatoka Nazareti akaja akakaa Kapernaumu mji ulioko pwani, mipakani mwa Zabuloni na Naftali; ili litimie lile neno lililonenwa na nabii Isaya, akisema, Nchi ya Zabuloni na nchi ya Naftali, njia ya bahari ng'ambo ya Yordani, Galilaya ya mataifa, watu wale waliokaa katika giza, wameona mwanga mkuu, nao waliokaa katika nchi na uvuli wa mauti mwanga umewazukia."*

Asingeweza kujitangaza mwenyewe.

Kwa kupigakelele au kulia katika mitaa. Isa. 42: 1-4, *"Nyamazeni mbele zangu enyi visiwan na mataifa wajipatie nguvu mpya na waje karibu wakanene; na tukaribiane pamoja kwa hukumu. Ni nani aliyemwinua mmoja atokaye mashariki ambaye katika haki amemwita mguuni pake? Ampa mataifa mbele yake na kumtawaza juu ya wafalme, awatowa wawe kama mavumbi kwa upanga wake, kama makapi yaliyopeperushwa kwa upinde wake. Awafuatia apita salama hata kwa njia asiyoikanyaga kamwe kwa miguu yake. Ni nani aliyetenda na kufanya jambo hilo, aviitaye vizazi tangu mwanzo? Mimi BWANA, wa kwanza na wa mwisho, mimi ndiye."*

Hii ilitimizwa wakati Yesu akijibu vitisho vya maisha yake. Math. 12:14-21, *"Lakini wale Mafsrisayo wakatoka wakafanya shauri juu yake jinsi ya kumwangamiza. Naye Yesu hali akiyafahamu hayo akaondoka*

huko na watu wengi wakamfuata akawaponya wote, akawakataza wasimdhihirishe; ili litimie neno lililonenwa na nabii Isaya, akisema, tazama mtumishi wangu niliyemteua; mpendwa wangu moyo wangu uliyependezwa naye; nitatia roho yangu juu yake, naye atawatangazia mataifa hukumu. Hatateta wala hatapaza sauti yake wala mtu hatasikia sauti yake njiani. Mwanzi uliyopondeka hatauvunja, wala utambi utokao moshi hatauzima, hata ailetapo hukumu ikashinda. Na jina lake mataifa watalitumainia."

Angeweza kuteseka kwa niaba yetu.

Alidharauliwa na kukataliwa na wanadamu.

- Isa. 53:1-3, *"Ni nani aliyesadiki habari tuliyoileta? Na mkono wa BWANA amefunuliwa nani? Maana alikuwa mbele zake kama mche mwororo, na kama mzizi kama nchi kavu; yeye hana umbo wala uzuri; na tumwonapo hana uzuri hata tumtamani. Alidharauliwa na kukataliwa na watu; mtu wa uzuni nyingi ajuaye sikitiko; na kama mtu ambaye watu hamficha nyuso zao, alidharauliwa wala hatukumhesabu kuwa kitu."*
- Yoh. 1:11, *"Alikuja kwa walio wake, na walio wake hawakumpokea."*

Mateso yake na kifo kwa ajili ya dhambi zetu.

- Isa. 53:4-6, *"Hakika ameyachukua masikitiko yetu, amejitwika huzuni zetu; lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, amepigwa na Mungu na kuteswa. Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ili kuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona. Sisi sote kama kondoo tumepotea, kila mmoja wetu ameigeukia njia yake mwenyewe; Na BWANA ameweka juu yake maovu yetu sisi sote."*
- Isa. 53:8, *"Kwa kuonewa na kuhumiwa aliondolewa na maisha yake ni nani atakayeisimulia? Maana amekatiliwa mbali na nchi ya walio hai; alipigwa kwa sababu ya makosa ya watu wangu."*
- Math. 8:17, *"Ili litimie lile neno lililonenwa na nabii Isaya, akisema, mwenyewe aliutwaa udhaifu wetu, na kuyachukua magonjwa yetu."*
- 1 Petr. 2:24, *"Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tuwe hai kwa mambo ya haki na kwa kupigwa kwake mliponywa."*

Alikuwa kimya mbele za waliomshitaki.

- Isa. 53:7, *"Alionewa lakini alinyenyekea, wala hakufunua kinywa chake, kama mwanakondoo apelekwaye machinjioni, na kama vile kondoo anyamazavyo mbele yao wakatao manyoya yake, naam, hakufunua kinywa chake."*

- Math. 27: 12-14, *"Maana kwa kunimwagia mwili wangu marhamu hiyo, ametenda hivyo ili kuniweka tayari kwa maziko yangu. Amin, nawambieni kila patakapohubiriwa injili hii katika ulimwengu wote tendo hilo alilolitenda huyu litatajwa pia kwa kumbukumbu lake. Wakati huo mmoja wa waleThenashara, jina lake Yuda Iskariote aliwaendea wakuu wa mkuhani."*

Kaburi lake na wenye dhambi na matajiri.

- Isa. 53:9, *"Waka mfanyia kaburi pamoja na wabaya; na pamoja na matajiri katika kufa kwake; ingawa hakutenda jeuri, wala hapakuwa na hila kinywani mwake."*

- Math. 27:38, *"Wakati uo huo wanyang'anyi wawili wakasulubiwa pamoja naye, mmoja mkono wake wa kuume na mmoja mkono wake wa kushoto."*

- Math. 27:57-60, *"Hata ilipokuwa jioni akafika mtu tajiri wa Arimathaya, jina lake Yusufu naye mwenyewe alikuwa mwanafunzi wa Yesu; mtu huyu alimwendea Pilato akamwomba mwili wa Yesu. Ndipo Pilato akaamuru apewe. Yusufu akautwaa mwili, akauzonga zonga katika sanda ya kitani safi. Akauweka katika kaburi lake jipya, alilokuwa amelichonga mwambani; akaviringisha jiwe kubwa mbele ya mlango wa kaburi, akaenda zake."*

Vyote ni kulingana na mapenzi ya Mungu, kwa ajili ya dhambi zetu.

- Isa. 53:10-12, *"Lakini BWANA aliridhika kumchubua; amemhuzunisha, utakapofanya nafsi yake kuwa dhabihu kwa dhambi, ataona uzao wake ataishi siku nyingi, na mapenzi ya BWANA yatafanikiwa mikononi mwake; ataona mazao ya taabu ya nafsi yake na kuridhika. Kwa maarifa yake mtumishi wangu mwenye haki, atawafanya wengi kuwa wenye haki, naye atayachukua maovu yao. Kwa hiyo nitamgawia sehemu pamoja na wakuu, naye atagawanya nyara pamoja na walio hodari; kwa sababu alimwaga nafsi yake hata kufa, akahesabiwa pamoja na hao wakosao, walakini alichukua dhambi za watu wengi, na kuwaombea wakosaji."*

- Matend. 2:23, *“Mtu huyu alipotelewa kwa shauri la Mungu lililokusudiwa na kwa kujua kwake tangu zamani ninyi mkamsulubisha kwa mikono ya watu wabaya, mkamwua.”*
- 1 Tim. 2:5-6, *“Kwa maana kuna Mungu mmoja na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu, mwanadamu Yesu Kristo, aliyejitoa dhabihu, kwa wote, utakaoshuhudiwa kwa majira yake.”*

Kupitia unabii huu wa kweli, Isaya alitabiri injili ya Masihi.

Angalia ambavyo Filipo alivyoweza kutumia vizuri “injili” ya Isaya katika kumhubiri Kristo.

Matend. 8:30-38, *“Basi Filipo akaenda mbio, akamsikia anasoma chuo cha nabii Isaya; akanena je yamekuelea haya unayosoma? Akasema nitawezaje kuelewa mtu asiponiongoza? Akamsihi Filipo apande na kuketi pamoja naye. Na fungu la maandiko alilokuwa akilisoma ni hili, aliongozwa kwenda machinjoni kama kondoo, na kama vile mwana kondoo alivyo kimya mbele yake amkataye manyoya, vivyo hivyo yeye naye hafunui kinywa chake. Katika kujidhili kwake hukumu yake iliondolewa. Ni nani atakayeeleza kizazi chake? Kwa maana uzima wake umeondolewa katika nchi. Yule towashi akamjibu Filipo, akasema, nakuomba nabii huyu asema maneno haya kwa habari ya nani; ni habari zake mwenyewe au za mtu mwingine? Filipo akafunua kinywa chake naye akianza kwa andiko lilo hilo, akamhubiri habari njema za Yesu. Wakawa wakiendelea njiani, wakafika mahali penye maji, Yule towashi akasema, tazama maji haya ni nini kinachnizuia nisibatizwe? [Filipo akasema ukiamini kwa moyo wako wote inawezekana, akajibu akanena, naamini ya kwamba Yesu Kristo ndiye mwana wa Mungu] akaamuru lile gari lisimame; wakatelemka wote wawili majini, Filipo na yule towashi; naye akambatiza.”*

Lakini unabii wa Isaya haukuwa tu kwa Masihi mwenyewe.

Kama jinsi Yesu alivyotangaza injili ya ufalme:

Marko. 1:14-15, *“Hata baada ya Yohana kutiwa gerzani, Yesu akaenda Galilaya, akiihubiri habari njema ya Mungu, akisema wakati umetimia na ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni na kuiamini injili.”*

Ndivyo alivyofanya Isaya katika unabii wake.

Injili ya ufalme

Habari njema kuhusu alikotokea.

Itakuja kupita katika "siku za mwisho".

Mlima wa nyumba ya Bwana itajengwa. Isa. 2:1-2, *"Hili ni neno alililoliona Isaya mwana wa Amozi katika habari za Yuda na Yerusalem. Na itakuwa katika siku za mwisho, mlima wa nyumba ya BWANA utawekwa imara juu ya milima, nao utainuliwa juu ya vilima na mataifa yote watauendea makundi makundi."*

Wakati huo ulitimizwa wakati Yesu alipoanza kuhubiri. Marko 1:14-15, *"Hata baada ya Yohana kutiwa gerezani, Yesu akaenda Galilaya akihubiri habari njema ya Mungu, akisema, wakati umetimia na ufalme wa Mungu umekaribia, tubuni na kuiamini injili."*

Itaanzia Yerusalemu.

Wakati neno likienea. Isa. 2:3, *"Na mataifa mengi watakwenda na kusema, njooni twende juu mlimani kwa BWANA, nyumbani kwa Mungu wa Yakobo naye atatufundisha njia zake nasi tutakwenda katika mapito yake katika sayuni itatoka sheria na neno la BWANA katika Yerusalemu."*

Kwa hiyo, Yesu anaeleza, neno lazima lienee kwanzia Yerusalemu. Luka 24:44-47, *"Kisha akawambia hayo ndiyo maneno yangu niliyowaambia nilipokuwa nikali pamoja nanyi, ya kwamba nilazima yatimizwe yote niliyoandikiwa katika torati ya Musa, na katika manabii na zaburi. Ndipo akawafunulia akili zao wapate kuelewa na maandiko. Akawambia ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu, na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake abari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu."*

Habari njema kwa uasili wake.

Utakuwa ni ufalme wa amani.

Watu hawatajifunza vita, mfalme wake atakuwa mfalme wa amani.

- Isa. 2:4, *"Naye atafanya hukumu katika mataifa mengi, atawakemea watu wa kabila nyingi nao watafua panga zao ziwe majembe na mikuki yao iwe miundu; taifa halitainua upanga juu ya taifa lingine, wala hawatajifunza vita tena kamwe."*
- Isa. 9:6-7, *"Maana kwa ajili yetu motto amezaliwa, tumepewa motto mwanamume; na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake; naye ataitwa jina lake mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, mfalme wa amani. Maongeo ya enzi yake na amani hayatakuwa na mwisho kamwe, katika kiti cha enzi cha Daudi na*

ufalme wake; kuuthibitisha na kuutegemeza kwa hukumu na kwa haki, tangu sasa na hata milele. Wivu wa BWANA wa majeshi ndio utakaotenda hayo."

Hivyo ufalme wa Mungu ni wa amani. Waru. 14:17, *"Kwa maana ufalme wa Mungu si nyama na kunywa, bali haki, na amani, na furaha katika Roho Mtakatifu."*

Hata mataifa nao watakuwemo.

Mataifa watamtafuta, ambapo kwa yeye watapata haki.

- Isa. 11:10, *"Na itakuwa katika siku hiyo, shina la Yese lisimamalo kuwa ishara kwa kabila za watu, yeye ndiye ambaye mataifa watamtafuta na mahali pake pa kupumzikia patakuwa na utukufu."*
- Isa. 42: 1, *"Tazama mtumishi wangu nimtegemezaye, mteule wangu ambaye nafsi yangu imependezwa naye, nimetia roho yangu juu yake; naye atawatolea mataifa hukumu."*
- Isa. 42:6, *"Mimi BWANA nimekuita katika haki, name nitakushika mkono, na kukulinda, na kukutoa uwe agano la watu, na nuru ya mataifa."*

Hivyo, Yesu amewaunganisha wote Wayahudi na Mataifa. Waef. 2:11-18, *"Maana yeye atakasye na hao wanaotakaswa wote pia watoka kwa mmoja. Kwa ajili hii haoni haya kuwaita ndugu zake akisema nitalihubiri jina lako kwa ndugu zangu, na tena nitakuwa nimemtumaini yeye. Na tena tazama mimi nipo hapa na watoto niliopewa na Mungu. Basi kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo ili kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti yaani ibilisi, awaache huru wale ambao kwamba maisha yao yote kwa hofu na mauti walikuwa katika hali ya utumwa. Maana ni hakika hatwai asili ya malaika ila atwa asili ya mzao wa Ibrahimu. Hivyo ilimpasa kufananananishwa na ndugu zake katika mambo yote, apatekuwa kuhani mkuu mwenye rehema, mwaminifu katika mambo ya Mungu, ili afanye suluhu kwa dhambi za watu wake. Na kwa kuwa mwenyewe aliteswa alipojaribiwa aweza kuwasaidia wao wanaojaribiwa."*

Habari njema kuhusu wakati wake wa baadaye.

Itakaa milele.

Hakutakuwa na mwisho katika ufalme wake. Isa. 9:7, *"Maongeo ya enzi yake na amani, hayatakuwa na mwisho kamwe katika kiti cha enzi cha Daudi na ufalme wake; kuuthibitisha na kuutegemeza kwa hukumu na kwa haki, tangu sasa na hata milele. Wivu wa BWANA wa majeshi ndio utakaotenda hayo."*

Ni kama jinsi malaika Gabrieli alivyomwambia Mariamu. Luka 1:31-33, *"Tazama utachukua mimba na kuzaa motto mwanamume; na jina lake utamwita Yesu. Huyo atakuwa mkuu ataitwa Mwana wa aliye juu, na Bwana Mungu atampa kiti cha enzi cha Daudi baba yake. Ataimiliki nyumba ya Yakobo hata milele, na ufalme wake utakuwa hauna mwisho."*

Itatawala katika mbingu mpya na nchi mpya, iliyoahidiwa na Mungu wakati ambapo Waisraeli watakapo ungana.

- Isa. 65:17-25, *"Maana tazama mimi naumba mbingu mpya na nchi mpya na mambo ya kwanza hayatakumbukwa; wala hayataingia moyoni. Lakini furahini, mkashangilie daima, kwa ajili ya hivi niviumbavyo, naam tazama naumba Yerusalemu uwe shangwe na watu wake wawe furaha. Name nitaufurahia Yerusalemu, nitawaonea shangwe watu wangu; sauti ya kulia haita sikika ndani yake tena wala sauti ya kuomboleza. Hatakuwapo tena motto wa siku chache, wala mzee asiyetimia siku zake kwa maana motto atakufa mwenye umri wa miaka mia, bali mtenda dhambi mwenye umri wa miaka mia atalaaniwa. Nao watajenga nyumba na kukaa ndani yake; watapanda mizabibu na kula matunda yake. Hawatajenga akakaa mtu mwingine ndani yake, hawatapanda akala mtu mwingine maana kama siku za mti ndivyo zitakavyokuwa siku za watu wangu na wateule wangu wataifurahia kazi ya mikono ya muda wa siku nyingi. Hawatajitaabisha kwa kazi bure, wala hawatazaa kwa taabu kwa sababu wao ni wazao wa hao waliobarikiwa na BWANA, na watoto wao pamoja nao. Na itakuwa ya kwamba kabla hawajaomba nitajibu, na wakiwa katika kunena nitasikia. Mbwa mwitu na mwana kondoo watalisha pamoja na samba atakula majani kama ng'ombe na mavumbi yatakuwa chakula cha nyoka. Hawata dhuru wala kuharibu katika mlima wangu mtakatifu wote, asema BWANA."*

- Isa. 66:22-23, *"Kama vile mbingu mpya na nchi mpya nitakazo fanya, zitakavyokaa mbele zangu asema BWANA, ndivyo uzao wenu na jina lenu litakavyokaa. Na itakuwa mwezi mpya hata mwezi mpya na sabato hata sabato, wanadamu wote watakuja kuabudu mbele zangu, asema BWANA."*

Ahadi hii ili kamiliswa kwa kuja kwake Masihi.

- 2 Petr. 3:10-14, *"Lakini siku ya Bwana itakuja kama mwivi katika siku hiyo mbingu zitatoweka kwa mshindo mkuu na viumbe vya asili vitaunguzwa na kufumuliwa na nchi na kazi zilizomo ndani yake zitateketea. Basi kwa kuwa vitu hivi vyote vitafumuliwa hivyo,*

imewapasa ninyi kuwa watu wa tabia gani katika mwenendo wa utakatifu na utauwa mkitazamia hata ije siku ile ya Mungu na kuihimiza, ambayo katika hiyo mbingu zitafumuliwa zikiungua na viumbe vya asili vitateketea na kuyeyuka? Lakini kama ilivyo ahadi yake, mnatazamia mbingu mpya na nchi mpya, ambayo haki yakaa ndani yake. Kwa hiyo wapenzi kwa kuwa mnatazamia mambo hayo, fanyeni bidii ili mwonekane katika amani kuwa hamna mawaa wala aibu mbele yake."

- Ufu. 21:1-4, *"Kisha nikaona mbingu mpya na nchi mpya kwa maana mbingu za kwanza na nchi ya kwanza, zimekwisha kupita, wala hapana habari tena. Name nikauona mji ule Mtakatifu Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu, umewekwa tayari kama bibi arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe. Nikasikia sauti kubwa kutoka katika kile kiti cha enzi, ikisema tazama maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao. Naye atafuta kila chozi katika macho yao wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena, kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita."*

Mwisho

Labda, tunaweza kuona ni kwa nini mitume na wengine walitumia Agano la Kale...

- Kuwashawishi wengi kwamba Yesu alikuwa ni Masihi.
- Kutangaza unabii kumhusu na ufalme wake ulikuwa unatimizwa.

Hatua yako ni nini kuhusu injili? Iliyotabiriwa na manabii karne nyingi kabla ya Kristo? Ilitangazwa na mitume na wahubiri katika karne ya kwanza, A.D.?

Maombi yangu na tumaini ni kwamba mtokeo yanaweza kuwa.....

Sawa na ile ya watu wa Samaria.

Matend. 8:12, *"Lakini walipoamini Filipo akihubiri mambo yanayohusu ufalme wa Mungu, na jina la Yesu Kristo walibatizwa wanaume kwa wanawake."*

Sawa na ile ya Towashi wa Kushi.

Matend. 8:30-38, *"Basi Filipo akenda mbio akamsikia anasoma chuo cha nabii Isaya akanena je yamekuelea haya unayosoma? Akasema nitawezaje kuelewa, mtu asiponiongoza? Akamsihi Filipo apande na*

kuketi pamoja naye. Na fungu la maandiko alilokuwa akilisoma ni hili, aliongozwa kwenda machinjioni kama kondoo, na kama vile mwana kondoo alivyo kimya mbele yake amkataye manyoya, vivyo hivyo yeye naye hafunui kinywa chake. Katika kujidhili kwake hukumu yake iliondolewa. Ni nani atakayeeleza kizazi chake? Kwa maana uzima wake umeondolewa katika nchi. Yule towashi akamjibu Filipo, akasema nakuomba nabii huyu asema maneno haya kwa habari ya nani, ni habari zake mwenyewe au za mtu mwingine? Filipo akafunua kinywa chake naye akianza kwa andiko lilo hilo, akamhubiri habari njema za Yesu. Wakawa wakiendelea njiani wakafika mahali penye maji, Yule Towashi akasema tazama maji haya; ni nini kinachonizuia nisi batizwe? Filipo akasema ukiamini kwa moyo wako wote, inawezekana, akajibu aknena, naamini ya kwamba Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu. Akaamuru lile gari lisimame, wakatelemka wote wawili majini, Filipo na Yule Towashi naye akambatiza."

Si kama baadhi ya walewaliokuwa Rumi, waliofanya mioyo yao kuwa migumu.

Matend. 28:23-31, *"Wakiisha kuagana naye siku, wakamjia katika nyumba aliokaa watu wengi sana, akawaeleza kwa taratibu na kushuhudia ufalme wa Mungu akiwaonya mambo yale Yesu, kwa maneno ya sheria ya Musa nay a manabii tangu asubuhi hadi jioni. Wengine waliamini yale yalionenwa, wengine hawakuyaamini. Na walipokuwa hawapatani wao kwa wao wakaenda zao Paulo alipokwisha kusema neno hili moja, ya kwamba Roho Mtakatifu alinena vema na baba zetu kwa kinywa cha nabii Isaya, akisema, enenda kwa watu hawa ukawaambie, kusikia mtasikia wala hamtafahamu; na kuona mtaona wala hamtatambua; kwa maana mioyo ya watu hawa imepumbaa, na masikio yao ni mazito ya kusikia, na macho yao wameyafumba wasije wakaona kwa macho yao, na kusikia kwa masikio yao, na kufahamu kwa mioyo yao, na kubadili nia zao nikawaponya. Basi ijulikane kwenu ya kwamba wokovu huu wa Mungu umepelekwa kwa mataifa nao watasikia! [alipokwisha kusema hayo, Wayahudi wakenda zao, wakiulizana mengi wao kwa wao.] Akakaa muda wa miaka miwili mizima katika nyumba yake aliyokuwa ameipanga, akawakaribisha watu wote waliokuwa wakimwendea, akihubiri habari za ufalme wa Mungu, na kuyafundisha mambo ya Bwana Yesu Kristo, kwa ujasiri mwingi, asikatazwe na mtu."*

Je mioyo yenu imefifia na masikio yakawa magumu kwa kusikia, kwamba habari njema ya ufalme na Bwana Yesu Kristo kwamba hawatowi jibu sahihi? Nadhani sivyo, nay a kwamba wote tuna sukumwa katika matendo mema na maneno haya ambayo Yesu aliongea mwanzo na mwisho wa kazi yake:

- Marko 1: 15, *".....Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia: tubuni na muiamini injili."*
- Marko 16:15-16, *".....Enendeni ulimwenguni kote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa."*